
## Kituo cha Kusajili/Kuandikisha Wanafunzi kipo

999 N. University Drive (Kaskazini mwa Mji)
Fort Worth, Texas 76114
Simu: (817) 815-7700
Faksi: (817) 815-7705
Barua pepe: spc@fwisd.org




**Programu za Lugha zinazoibuka**

Dr. Marie Mendoza
Mkurugenzi Mkuu
marie.mendoza@fwisd.org

**Student Placement Center**
**(Kituo cha Kupanga wanafunzi)**

Diana De La Paz
Mkurugenzi
diana.delapaz@fwisd.org

**Wasimamizi wa mashule ya Fort Worth yani Fort Worth Independent School District hawabagui mtu yeyote kwa msingi wa rangi ,asili, dini, eneo, Jinsia,ulemavu, chaguo ya kijinsia , umri, ikiwa wako kwenye jeshi au la, kwa programu na shughuli zao. Mtu/Watu wafuatao wamepewa kazi ya kushughulikia maswala yote yanayohusu sheria zetu za kuzuia ubaguzi: Patricia Sutton, 215 NE 14th Street, Fort Worth, TX 76164, Director of Special Services, 817.814.2458, Cynthia Allen, Title IX Coordinator, 7060 Camp Bowie Blvd, Fort Worth, TX 76116, 817-814-1830, Email: TitleIX@fwisd.org**

Fort Worth
INDEPENDENT SCHOOL DISTRICT
www.fwisd.org

Rev. 2/4/25

Swahili




# Kituo cha Kusajili/Kuandikisha Wanafunzi

Fort Worth ISD

## Kituo cha Kusajili Wanafunzi ni nini?

Kituo cha Kusajili Wanafunzi kinawasaidia wanafunzi ambao ni wageni kwa Wilaya ya Shule za Fort Worth ISD ambao kwa kawaida wanazungumza au kusikia lugha nyingine isipokuwa Kiingereza, nyumbani mwao kujiandikisha shuleni. Ofisi hiyo inatoa huduma nyingi kwa wanafunzi wapya na familia zao.

## Je, wanafunzi wote wapya wanaozungumza lugha nyingine isiyo Kiingereza ni lazima wafanye mtihani?

Endapo kuna lugha nyingine isiyo Kizungu kwenye maswali yoyote hapo chini NA hujawahi kujiunga na shule yoyote ya Texas, basi jibu ni "Ndiyo". Wanafunzi ambao kwa kawaida wanazungumza au kusikia lugha nyingine isiyo Kizungu nyumbani mwao NA ni wageni Texas wanahitaji kufanyishwa mtihani.

1. Je, ni lugha gani inayotumika nyumbani mwa mtoto **mara mingi**?
2. Je, ni lugha gani anayotumia mtoto **mara mingi**?
3. Ikiwa mtotoalikuwa anaishi nyumbani na familia, ni lugha ipi ilitumika sana? Ikiwa mwanafunzi hakuwa na nyumbani au familia jibu LA

## Shughuli hii yote inachukua muda gani?

Utachukua kati ya dakika 45 hadi masaa 2.5, ikitegemea na umri wa mwanafunzi na aina ya mtihani inayohitajika ili kuhakikisha mwanafunzi anaingizwa kwenye programu inayomfaa zaidi. Wazazi, ambao watoto wao wamefikia umri wa kuanza shule ya msingi, wanaweza kupangiwa asubuhi mwishoni au mchana, kwa sababu mtihani hizi si kubwa kama zile za wanafunzi wakubwa kiumri.

## What records pertaining to the student should parents bring to the Student Placement Center?

- Ushahidi wa umri na utambulisho wa Mwanafunzi.
- Rekodi za chanjo za hivi karibuni.
- Kitambulisho cha mzazi au mlezi.
- Dhibitisho ya kuonesha mahali unapoishi.
- Ripoti za shule ulizo kuwamo awali, au rekodi yoyote ya kuonesha ya shule uliyokuwa kitambo.
- Mkarakatasi ya kuonesha kwamba wewe ni mkimbizi na umepewa makao rasmi nchini.

Wazazi wanaweza kutuma makaratasi zinazohitajika kwa baruapepe au faksi.
**Baruapepe: spc@fwisd.org**
**Faksi: 817.815.7705**

## Je, wazazi wanatakiwa kupiga simu kupanga mkutano?

**Ndiyo, wazazi watapigiwa simu na mfanyakazi wa SPC ili kupanga mkutano.**

## Saa za kazi ni zipi?

Katika kipindi cha masomo shuleni, Kituo cha Usajili cha Wanafunzi kinafunguliwa kuanzia saa 2:30 asubuhi hadi saa 10:30 jioni. Jumatatu-Ijumaa, isipokuwa kwa siku za likizo za shule.

## Je, wazazi watarajieie nini wanapowaleta watoto wao kituoni?

Wazazi watarajie:

- kupokelewa na wafanyakazi wanaozungumza Kiingereza, Kihispaniola, na lugha zingine (wakalimani watakuwepo ukituma ombi)
- Kupokea usaidizi na habari kuhusu
  - Usajili/Uandikishaji wa wanafunzi
  - Mtihani wa kwanza kabla ya kupewa nafasi shuleni
  - Habari kuhusu lugha zaidi ya mojana program za ESL.
  - Tafsiri ya kimataifa ya ripoti za shule
  - Habari kuhusu usafirishaji wa wanafunzi.
  - Habari kuhusu chanjo.
  - Habari za Fort Worth ISD kuhusu mavazi , kompyuta ya wazazi na kadhalika.information.
  - Mafunzo kuhusu shule kwa wazazi na wanafunzi wapya.
  - Huduma za kisheria.
- kuondoka Kituoni wakiwa na bahasha ya manjano/yellow inayobeba taarifa za kujiunga kwa shule waliyopewa)
- huduma za usaidizi kufuatilia kama vile kutembelea shule husika, kutafsiri makaratasi za lugha geni, kusaidia kwa masuala ya usafiri na kutembelea nyumbani, kama inavyotakiwa

## Je, kuna malipo kwa huduma zinazotolewa na kituo hiki?

Hapana, Fort Worth ISD inatoa huduma hizi bila malipo yoyote kwa mzazi.